

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**  
**HALMASHAURI YA WILAYA LUSHOTO**  
**SHULE YA SEKONDARI SHAMBALAI**  
**S. L. P 52, LUSHOTO-TANGA**



Kumb.Na: **SSS/S/JOINIST/I/2021/1**  
**MZAZI/MLEZI WA**

---

---

**FOMU YA MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA**  
**MWAKA 2021 KATIKA SHULE YA SEKONDARI SHAMBALAI**

**SEHEMU A:**  
**UTANGULIZI**

1. Hongera kwa kuchaguliwa kujiunga na Kidato cha kwanza mwaka 2021 katika shule ya Sekondari Shambalai iliopo kata ya Lushoto mjini, Wilaya ya Lushoto Mkoa wa Tanga.
2. Ukiwa Shambalai Sekondari, utalazimika kufuata Sheria, Kanuni na Taratibu za Shule.
3. Utatakiwa kukamilisha **kiambatanisho A na B**.
4. Utaripoti shuleni tarehe **11/01/2021** bila kuchelewa, hivyo mwananfunzi ataripoti shuleni akiwa na mzazi/mlezi katika ofisi ya Mkuu wa shule Jengo la Utawala.
5. Fika na nakala ya cheti cha kuzaliwa, kama huna cheti cha kuzaliwa, nenda Mahakamani ili **Uape upewe Affidavit**, itakayo kutambulisha kuwa wewe ni raia wa Tanzania.

**SEHEMU B:**  
**VIFAA VYA DARASANI**

1. Ufike na daftari 12 kwa ajili ya masomo ya darasani aina ya Counter Book, Kalamu ya wino wa bluu/nyeusi, Mkebe, Pencil, Ruler, Begi la shule na vifaa vingine vinavyoruhusiwa kitaaluma.
2. Dictionary (Kamusi) ya Kingereza kwa Kiingereza

- Karatasi binafsi za kujibia mitihani aina ya Rim paper A4 zitunzwe na mzazi kwa ajili ya Mitihani na majaribio ya kila wiki, mwezi n.k.

**SEHEMU C:  
SARE YA SHULE**

NA.	SARE/MAHITAJI	MAELEZO
	Mashati 2 meupe ya Mikono Mifupi, Tetroni(Lisiwe linalo bana au linalo oneshwa ndani)	Anunue duka lolote.
2	Suruali 2 ndefu za heshima za rangi ya kaki zenye malinda za kitambaa kizito kisichooneshwa ndani. <b>Mshono wa chupa au model hauruhusiwi.</b> (Kwa Wavulana)	Anunue/Ashone duka lolote.
3	Masweta 2 ya rangi ya Bluu.	Anunue duka lolote.
4	Viatu vyeusi vya ngozi jozi 2 vya kufunga na kamba ( <b>visiwe buti au vyenye visigino virefu</b> ), na <b>soksi nyeupe.</b>	Anunue duka lolote.
5	Mkanda wa kuvalia suruali mweusi wa ngozi	Anunue duka lolote.
6	Soksi nyeupe jozi mbili.	Anunue duka lolote.
7	T-shirt Dack blue zinapatikana shuleni kwa shilingi elfu kumi 10,000/=	Anunulie Shule
8	Sketi nyekundu ndefu, yenye marinda, isiwe na Mkanda Mpana na isiwe fupi. Suruali haziruhusiwi (Kwa wasichana)	Anunue duka lolote.
9	Shati jeupe mikono mirefu hijabu nyeupe ndefu inayositiri mwili. (Kwa wasichana)	Anunue duka lolote.

**MUHIMU:**

- Ukifika shuleni ripoti moja kwa moja kwa Mkuu wa Shule kisha taratibu nyingine zitafuata.
- Mwanafunzi hataruhusiwa kuleta/kuvaa vazi la aina yeyote isipokuwa sare za shule na T- shirts za shule kwa siku ya Ijumaa.
- Hakikisha unasoma kwa makini maelezo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

*KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI SHAMBALAI*

.....  
**SELESTINA L. IFANDA**  
**Mkuu wa Shule**

**SIMU: 0788-340031/ 0764-260023.**

**Kiambatanisho A**

**OFISI YA RAIS-TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
SHULE YA SEKONDARI SHAMBALAI**

**Ajaze Mwanafunzi**

1. Jina Kamili.....
  2. Tarehe ya Kuzaliwa.....
  3. Uraia.....
  4. Dini.....
  5. Shule ya Msingi uliyosoma.....
- Saini ya mwanafunzi.....

**Maelezo Binafsi ya Mzazi/Mlezi:**

- a) Jina la Baba ..... saini.....  
Kazi afanyayo.....  
Anwani ..... Simu.....
- b) Jina la Mama ..... saini.....  
Kazi afanyayo.....  
Anwani ..... Simu.....

**NB: Iwapo wazazi hawapo jaza taarifa za mlezi:**

- c). Jina la mlezi..... saini.....  
Anwani ..... Simu: .....

Naahidi kwamba sitampa simu mwanafunzi anapokuja shuleni kwakuwa natambua kuwasimu haziruhusiwi kwa mwanafunzi. Hivyo akipatikana na simu shuleni anastahil iafukuzwe shule na nipo tayari kwa hilo.

Mimi..... Baba/Mama/Mleziwa.....

Saini ..... Tarehe.....

**Kiambatisho B**

*The united Republic of Tanzania*

**President Office - Regional Administration and Local Government**

Shambalai Secondary School

P.O BOX 52

Lushoto

Date:.....

Ref. No. SSS/S/HOSP/I/2021/1

To the Medical Officer

.....,

.....,

.....

**Ref: A PUPIL'S MEDICAL EXAMINATIONS FORM**

Please, examine the Student..... in respect of these areas and any other area(s) deemed fit Please. Delete whichever applies.

Does the Pupil have problems in connection with...?

a) Sight Yes/No. If yes, state.....

b) Hearing. Yes/No. If yes, state .....

c) T.B or any other Chronic Diseases. Yes/No. If yes, state.....

.....

d) Blood Pressure. Yes/No. If yes, state .....

.....

e) Any Physical Impairment(s). Yes/No. If yes, state .....

.....

Do you therefore recommend this pupil to pursue studies at this school?

.....

Name.....Signature.....Date.....

Official Title..... Official Stamp.

*Jamhuri ya Muungano wa Tanzania*  
**Ofisi ya Rais –Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa**  
**Shule ya Sekondari Shambalai S.L.P 52, Lushoto.**  
**Sheria na Kanuni za Shule**

**1. HESHIMA**

- a) Mwanafunzi atasimama kumsalimia Mwalimu au mtu yoyote aliyemzidi umri anapopita ,anapoingia darasani au kwenye ukumbi wa mikutano.
- b) Mwanafunzi atatumia lugha safi (inayokubalika) wakati wowote kati yake na wenzake na kwa watu wengine akiwa shuleni au nje ya shule.
- c) Mwanafunzi anatakiwa kuwaheshimu wafanyakazi wote walioko shuleni kama walezi wake.
- d) Mwanafunzi ataitika wito mara moja na kukimbilia aliko Mkuu anayemwita.
- e) Mwanafunzi anapaswa kuheshimu kazi yeyote anayopewana Mwalimu au Mlezi na anatakiwa ashirikiane na wenzake ili kuifanya kazi hiyo.
- f) Mwanafunzi anaakiwa kuheshimu Bendera ya Taifa na picha za viongozi wa serikali, nembo ya Taifa, wimbo wa Taifa na fedha za Taifa.
- g) Mwanafunzi atasimama katika mstari wakati wowote anaposubiri kupata huduma/maelekezo yeyote.
- h) Mwanafunzi atakaa kimya wakati wowote akiwa darasani, asitoke nje ya darasa au eneo la shule bila ruhusa ya Mwalimu. Atatoka nje ya eneo la shule kwa siku zilizo tangazwa au ruhusa maalumu.

**2. MAHUDHURIO**

- a) Mwanafunzi anatakiwa ahudhurie vipindi vyote vya darasani kwa muda wote wa masomo. Inapotokea mwanafunzi akashindwa kufika shuleni kwa sababu yeyote ile, mzazi/mlezi afike kutoa taarifa kwa mmoja wapo kati ya wafuatao;-:
  - i. Mwalimu wa zamu wiki hiyo.
  - ii. Mwalimu wa darasa.
  - iii. Makamu wa Mkuu wa Shule.
- b) Mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria mikutano yote ya shule kama vile Baraza la Shule,Ukaguzi wa usafi na Kupandisha Bendera ya Taifa.
- c) Mwanafunzi atatakiwa kuwahishughulizoteshulenika mazilivyopangwakwenyeratibayas hule.Tena anatakiwa kuwahanapotakiwa au anaposikiakengele.
- d) Mwanafunzi anatakiwa kufanya mazoezi, majaribio na mitihani yote anayopewa na Mwalimu wa somo darasani. Akikosa jaribio au mtihani wowote, akamuone Mwalimu wa somo na Mwalimu Mwandamizi Taaluma kwa ajili ya kupewa mtihani/jaribio la kufanya.

**3. SARE YA SHULE NA USAFI**

Mwanafunzi anatakiwa kuwa katika sare safi ya shule wakati wote wa saa za shule. Atatakiwa kuvaa vazi tofauti pale tu atakapo agizwa kama vile nguo za michezo wakati wa michezo.

## **MAKATAZO**

### **4. SEHEMU ASIZORUHUSIWA KUTEMBELEA MWANAFUNZI**

- a) Mwanafunzi asitembeleese hemuzifuatazo isipokuwa wakibali au ruhusa:
  - i. Ofisi ya Walimu.
  - ii. Maabara.
  - iii. Nyumbaza Walimu na Wafanyakazi.
  - iv. Chumba cha Walimu au Wafanyakazi
- b) Mwanafunzi haruhusiwi kabisa kutembelea sehemu hizi:
  - i. Vilabu vya pombe
  - ii. Nyumba za starehe
  - iii. Nyumba za kufika wageni
- c) Mwanafunzi haruhusiwi kutoka nje ya eneo la shule bila ruhusa/kibali maalumu.

### **5. MARUFUKU:**

- a) Kuiba mali ya mtu binafsi au umma.
- b) Kufanya uasherati, ubakaji au ushoga.
- c) Kulewa kilevi cha aina yeyote au kuvuta sigara au bangi.
- d) Kupiga au kupigana.
- e) Kuharibu mali ya umma.
- f) Kuoja au kuolewa.
- g) Mwanafunzi kumiliki/kuwa na simu ya mkono ni popote.

### **6. MAKOSA YANAYOFUKUZISHA SHULE:**

- a) Uasherati, ubakaji na ushoga, kuoja au kuolewa.
- b) Wizi, ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya.
- c) Kuvuta bangi.
- d) Kupiga au kupigana.
- e) Kudharau Bendera ya Taifa, kuharibu mali ya umma.
- f) Kupata, kutoamimba au kusababisha mimba au njeyashule.
- g) Kugoma, kuongoza, kuchochea mgomo au vurugu, kuchafua amani au usalama wa watu.
- h) Kukashifu na kukataa adhabu halali.
- i) Kukutwa na simu ya mkononi.

### ***Angalizo:***

Ni jukumu la mwanafunzi kufuata sheria nataratibu zilizowekwa pamoja na nyingine ili kuepuka adhabu nakufukuzwa shule.

Walimu shuleni ni waelekezaji, walezi, waelimishaji na washauri. Mwanafunzi akiwa sikiliza, atafika kule anako tarajia/alikopanga afike.